- kuiga watu wazima na wenzi wa kucheza, na
- kucheza vizuri na sesere, wanyama, na watu.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MIAKA MINNE

Watoto wenye afya baada ya miaka minne wanaweza:

- kutumia sentensi ya maneno tano au sita,
- kufuata maagizo yenye hatua tatu ("vaa nguo. Chanua nywele yako. Sugua meno yako, na osha uso yako"), na
- kushirikiana na watoto wengine.

DALILI ZA MTOTO ANAYEKUA POLEPOLE NI ZIPI?

- Ukosefu wa kukua kimwili
- Utapiamlo
- Mifupa dhahifu
- Kutokuona vizuri
- Usununu
- Uzani wa chini
- Kupoteza kusikia

UNAPASWA KUZUNGUMZA NA NANI IKIWA MTOTO WAKO HAKUI KWA MWENDO MZURI UNAOFAA?

Ikiwa una wasiwasi kuhusu jinsi mtoto wako anavyokua tafadhali zungumza na daktari wa mtoto wako. Hakikisha umempeleka mtoto wako kuangaliwa mara kwa mara, na kwa chanjo.

Kwa habari zaidi kuhusu kukua kwa mtoto kwenye wavuti, tafadhali tembelea:

www.cdc.gov/ncbddd/autism/ActEarly

www.nidcd.gov/health/voice/speechandlanguage

• • •

Brosha hii ilitengenezwa na usaidizi wa habari na rasilimali kutoka:

National Center for Birth Defects and Developmental Disabilities

Centers for Disease Control

Brosha hii ilitengenezwa na ufadhili kutoka kwa Idara ya Afya na Ofisi ya Huduma za Wanadamu ya Kuwapatia Wakimbizi makazi mapya.

HABARI YA MAWASILIANO:
riht@uscridc.org
U.S. Committee for Refugees and Immigrants
1717 Massachusetts Ave., NW
Suite 200
Washington, DC 20036
Simu: 202 • 347 • 3507
Faksi: 202 • 347 • 7177
www.refugees.org

Kuangalia Mtoto Wako Akikua

(Hatua za Kukua)

Watching Your Child Grow

(Development Milestones)

(Swahili)

U.S. COMMITTEE FOR REFUGEES AND IMMIGRANTS

USCRI

www.refugees.org

Protecting Refugees, Serving Immigrants, Upholding Freedom since 1911

KUMWANGALIA MTOTO WAKO AKIKUA

Miaka ya kwanza ya maisha ya mtoto wako ni wakati muhimu kwao kukua kimwili, kimhemko, na kijamii. Hii inaitwa kukua kwa mtoto. Kuna viwango tofauti vya kukua kwa mtoto ambavyo wazazi wanaweza kufuata ili kuona kama mtoto wao anakua kwa kiwango kizuri. Nchini Merikani, wazazi wanashauriwa kuangalia kila mara jinsi akili, macho, masikio na maungo yanavyokua ili kuangalia dalili zozote zisizofaa.

NI NINI NINACHOSTAHILI KUGUNDUA KUHUSU MTOTO WANGU?

Watoto hukua vitofauti katika hatua zao za kukua. Kila mtoto hukua kwa wakati wake, na mtoto wako anaweza kufikia hatua hizi kabla au baada ya watoto wengine waliyo na umri sawa. Brosha hii ni mwongozo rahisi wa kukusaidia kuelewa kukua kwa mtoto na unachostahili kumuuliza daktari wa mtoto wako ikiwa una wasiwasi. Hapa kuna baadhi ya dalili ambazo mzazi anastahili kuangalia wakati mtoto wake anapokua akikua.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MIEZI SABA

Kabla ya mwisho wa miezi saba, watoto wengi wenye afya wanaweza:

- kupindua kichwa wakati jina lao linapoitwa,
- kuchekea mtu mwingine,
- kuitikia sauti na masauti,
- kufurahiya kucheza kijamii,
- kuweza kushika sesere ndogo, na
- kufuata vitu /mwangaza unaosonga karibu na macho.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MWAKA MMOJA (MIEZI 12)

Watoto wenye afya baada ya mwaka mmoja wanaweza:

- kutumia konyeza za kawaida (kupunga kwaheri).
- kutoa sauti rahisi,
- kuiga vitendo anapokuwa akicheza (kupiga makofi), na
- kuitikia wakati anapoambiwa “hapana”.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MWAKA 1 1/2

Watoto wenye afya baada ya mwaka 1 1/2 wanaweza:

- kufanya vitendo rahisi vya kujifanya (kuongea kwa simu ya sesere),
- kunyooshea kidole vitu vinavyopendeza,
- kuangalia kitu wakati unaponyoosha kidole na kusema “angalia”, na
- kutumia maneno kadhaa kivyao.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MIAKA MIWILI

Watoto wenye afya baada ya miaka miwili wanaweza:

- kutumia sentensi ya maneno mawili,
- kufuata maagizo rahisi,
- kupendezwa na watoto wengine, na
- kunyooshea kidole kitu au picha inapotajwa.

KUKUA NA MAENDELEO BAADA YA MIAKA MITATU

Watoto wenye afya baada ya miaka mitatu wanaweza:

- kubusu au kukumbatia watoto wengine,
- kutumia sentensi ya maneno mawili,